






SIKILIZA RADIO MITIKI 91.5 IJUMAA 1:30JIONI AU JUMAMOSI 8:00 MCHANA

KVTC TANGU 1992

# Kutoka Dawati la Irvine

**CORONA INAUWA, OSHA MIKONO MARA KWA MARA**

Toleo hili ni special kwasababu lina ushuhuda wa mafanikio ya KVTC kutoka kwa waasisi wa KVTC, hivyo nimewaachia nafasi ili waweze kutukumbusha tulipotoka.

## KVTC-Miaka ya Mwanzo

Na Crispin Goldin

KVTC ilijulikana kama Mitiki na ilianzishwa miaka ya 1990 ambao ni mchango wa juhudi za Tony Fraser (Mwakilishi wa Kitengo cha Maendeleo Jumuiya ya Madola yaani CDC ambao pia ndio waliokuwa wafadhili) na Mtanzania Bwana Misitu Fabian Nyaki ambao kwa pamoja walitafuta ofisi, jenga nyumba, waliajiri, na kufanya majadiliano na viongozi wa serikali na wenyeji juu ya upatikanaji wa ardhi bora ya kupanda Mitiki. Ni uongozi wao ulioanzisha Kampuni na safari hii ndefu inayoendelea mpaka leo.



Nilijiunga na Kampuni mwaka 1996 na nilihusika na endeshaji wa shughuli za Kampuni. Kwangu ulikuwa wakati wa pekee kwasababu wafanyakazi walikuwa wana moyo na pamoja tuliweza kupanda mamilioni ya Mitiki. Kampuni ilikuwa imegawanywa kwenye Wilaya mbili, Kilombero upande wa Kaskazini chini ya Bwana Nyaki na Bwana Mteweli na Masota na upande wa Ulanga chini ya Bw. Hamisi, Bw. Mahengo, Bw. Ngenuko na Bw. Kahamba. Ofisi yetu ilikuwa Kibaoni na kulikuwa na ofisi ndogo katikati ya Narubungo na Mafinji. Kila upande ulikuwa una bustani ya miche (Luhusa) na karakana na stoo vilikuwa Kibaoni na Kiwanda cha kuchakata kilikuwa ni wazo la mbali sana. Bila kusahu, hakukuwa na daraja wakati huo hivyo kuruka kwenda Ulanga inamaanisha kupanga kuendana na ratiba ya kivuko la utalala upande uliopo mpaka asubuhi. Hizi zilikuwa pia zama za kutokuwepo simu za mkononi! Mabwana misitu wa sasa wanaweza kupata picha hiyo? Tulikuwa na mawasiliano ya radio na simu au fax za sateliti mabayo inagharimu dola 6 kwa dakika, na watu wa kituo cha utafiti cha Ifakara walikuwa wanaiona kama mkombozi hasa wakiwa na ujumbe wa haraka wa kutuma Ulaya. Barua pepe na mtandao vilikuwa ni ndoto! Siku za mwanzo tulikuwa tunapanga mikakati ya kilimo cha miti, matumizi bora ya ardhi na kuchagua maeneo ya kupanda, tulikuwa na timu inayohusika na barabara (Kibuga), kuchagua maeneo (Shija), jamii (Haule), tafiti (Mabuza) na ramani (Speedo). Kuna wengine lakini nimewasahau, kwa ujumla ilikuwa ni team nzuri na inayojituma



## Miaka 20 ya Maajabu

Na David Parkhill

KVTC niliyoanza nayo mwaka 2000 ni tofauti na KVTC ya sasa, na ninafuraha kuhusishwa na maendeleo ya Kampuni kwa miaka zaidi ya 20. Miaka ya 2000 KVTC ilikuwa inaendeshwa kama ofisi ndogo ya TANWAT hivyo Mkurugenzi na Mkuu na Mkuu wa Kitengo cha Misitu walikuwa wanakaa Njombe, wakati Ifakara alikuwepo Meneja wa Mradi na Meneja Mtaalamu. Team ya Ifakara Ilikuwa ndogo maana kazi kubwa ilikuwa ni kuandaa maeneo na kupanda miti.



Nimeona mabadiliko makubwa kutoka kipindi kile: Kuingia kwa FinnFund kama muwekezaji mdogo na kuondoka kwa Maendelo ya Jumuiya ya Madola (CDC); ujenzi wa kiwanda cha kuchakata Magogo; na kampuni kujiendesha kibiashara;utaalamu mkumbwa tulioupata wa kupanda Mitiki tangu kipindi ambacho mwanzoni ilikuwa kama majaribio tu; Kuwa na ndege kutoka Ifakara kwenda Dar es Salaam na kurudi; na urahisishwaji shughuli kutokana na ujenzi wa Daraja la Kilombero badala ya kivuko; na mwisho KVTC kuanza kutengeneza faida.

# Mabadiliko 1992 Mpaka 2020

Na Tony Finch

Wawekezaji wametumia zaidi ya dolla za kimarekani milioni 50 ndani ya miaka 25 kuanzisha shamba la Mitiki hekari 8000 na kujenga kiwanda cha kisasa cha kuchakata mbao na kuongeza thamani ya mbao na kuwa Kampuni kubwa ya Mitiki Afrika na wasafirishaji njee wakubwa wa mbao za Mitiki.Wamewezaje haya kulinganisha na kilichotarajiwa na wawekezaji wa Jumuiya za Madola (CDC)?

Kuna mabadiliko mbalimbali yaliyotokea tangu wazo lilopendekezwa miaka 27 iliyopita la kuanzisha biashara ya Mitiki. Mabadiliko haya ni kwenye upande wa kiutaalamu na kijamii. KVTC imefanikiwa kwenye upandaji miti zaidi hata kuliko waanzilishi walivyotegemea.

Mradi haukuwa na makuu au mambo mengi zaidi ya kutaka kupanda mitiki kibiashara na haukuwa umepanga kuwa na kiwanda cha uchakataji magogo. Mwanzoni walifanya tafiti na kuchukua sampuli ya mbao ya Mitiki kutoka Mtibwa Morogoro na kutuma Denmark ambapo ilipatiwa makadirio ya dollar za kimarekani 2000 kwa mita za ujazo (USD 2000/cu.m). Wakati huo bado usafirishaji wa Magogo njee ya nchi ulikuwa unarushusiwa na kulikuwa na soko la nguzo za simu. Na kwa kuwa kwenye soko la dunia mrahaba mmoja wa gogo ulikuwa ni juu ya dolla 300 kwa mita za ujazo, hivyo basi biashara ilionekana kama itakayoweza kuwa na mafanikio, na ndipo CDC wakaamua kuwekeza.

Mitiki inakuwa sehemu nyingine za Tanzania (ukiachia bonde la Kilombero) lakini hakukuwa na ardhi/eneo la kupanua kilimo cha Mitiki sehemu hizo. Mashamba sehemu nyingine Tanzania yalikuwa ni ushuhuda tosha juu ya mafanikio yanayoweza kuletwa na upandaji Mitiki. Ifakara na maeneo yanayozunguka kulikuwa na ushahidi mdogo mdogo unaonyesha kwamba Mitiki inaweza kustawi. Na kwa baadhi ya wakulima waliona kama Mtiki ni "Mti wa Pesa" kwasababu waliweza kuuza miti ya miaka 10 mpaka 15.

Kuna vitu viwili vya kuangalia kwenye upandaji Mitiki: moja ni urefu wa miti na eneo la ardhi lenye miti (basal area). Eneo la ardhi lenye miti liliwekwa ±20 mwanzoni badala ya ±16 ambayo huwa inatumika kiuhalisia. Kiwango hiki cha basal area ni kiwango cha makadirio ya juu na inamaanisha tulitegemea mavuno kwa hekari kuwa juu. Pia tulitegemea kuweza kupanda hekari 10,000 kutokana na tathimini ya awali lakini ardhi iliyokuwa inafaa Mitiki ilikuwa ni hekari 8,000 tu hivyo kushusha mategemeo yetu.

Vitu vitatu vilifanyika kurekebisha haya mapungufu yaliyotajwa hapo juu:

1. Kuanzisha kiwanda cha uchakataji Magogo madogo na kutafuta soko India na ndani ya nchi;
2. Kuanzisha tafiti mwaka 2013 ili kuweza kuongeza uzalishaji;na
3. Kuanzisha program ya wakulima wa njee wanaofikia hekari 2,000 zikimilikiwa na wakulima 1,000

Mikakati hii haikupangwa kwenye tathimini za awali lakini imesaidia kuongeza ufanisi wa kampuni kiuchumi. Mabadiliko mengi yametokea duniani tangu kuanzishwa kwa KVTC na la karibuni kabisa ni adhari za ugonjwa wa virus vya CORONA. Lakini, tofauti na biashara nyingine duniani, miti ya KVTC itaendelea kukua na kuongezeka thamani hata kama uzalishaji utasitishwa kwa miezi 12 au zaidi. Upigaji marufuku usafirishaji njee wa magogo ya mitiki, na matokeo ya kuja kwa simu za mkononi na kuuwa biashara ya nguzo za simu bado havikuathiri uchumi wa KVTC. KVTC imeleta matokeo ya kimaendeleo, kiuchumi na kijamii kwenye bonde la Kilombero na kuweka rekodi nzuri na ambayo itaendelea zaidi ya miaka 25 tena mbele.

# Hali Murua ya Mitiki

Na Kennedy Haule

Ninajivunia kuwa mmoja wa waasisi wa KVTC. Nusu karne imepita na mambo mengi yametokea, na shikamoo zikiambatana na umri na mvi kichwani mwangu. Kumetokea mabadiliko mengi, kiuchumi,kijamii na kimazingira toka KVTC ilipoanzishwa. Kazi yakwanza ambayo niliifanya kwa miezi sita ya mwanzo kama Surveyor ni kutafuta maeneo bora yakupanda mitiki kulingana na aina ya uoto, udongo na mazingira. Mwanzoni KVTC haikuwa imetambua tofauti ya udongo kwenye ukuaji wa Mitiki hivyo ilikuwa inapata matokeo tofauti ya ukuaji hata kama utunzaji unafanana. Baada ya kumaliza shahada ya pili Norway nilirudi KVTC na kuanza kuchunguza tofauti ya ukuaji mitiki kwenye udongo wa aina mbali mbali. Tuligundua kuna aina tano za udongo na tuliweza kupata maeneo ya Mitiki inapokuwa vizuri na matokeo yake tukaanza kupanda kwa kulingana na maeneo maalumu yaliyochaguliwa na tukaanza kuona matokeo chanya ya ukuaji. Tathimini ya awali iliyofanyika na CDC na serikali ya Tanzania iliona kuwepo kwa eneo zuri kwenye bonde la Kilombero kwa ajili ya kilimo cha Mitiki lakini sio maeneo yote yanayokuwa Mitiki vizuri. Hivyo tuligundua eneo letu linalofaa Mitiki ni hekari zaidi kidogo ya 8,000 na kwamba matarajio ya awali ya kupanda hekari 10,000 kama ilivyotarajiwa haitawezeakana. Juhudi za kuendelea kutafuta ardhi bora ili kufikia malengo zilishindikana na hivyo ilipofika mwaka 2010 tuliweza kupanda eneo lote linalofaa na eneo lilobaki linahifadhiwa kwa ajili ya utunzaji bioanuwai, vyanzo vya maji na viumbe vingine.



# Mapinduzi -Mfuko wa Jamii

Na Kennedy Haule

Mwaka 2000 mahusiano yetu na jamii hayakuwa mazuri, na kulikuwa na malalamiko kwamba KVTC haifanyi vya kutosha kwenye jamii inayoizunguka. Kulikuwa na umbea kwamba Mitiki inaleta jangwa na inakausha maji. Kilimo cha miti kilikuwa ni jambo ngeni kwa watu: wanajiuliza inakuwaje miti inayopunguzwa shambani kuachwa tu na kuozea shambani (wakimaanisha upunguziaji miti usionafaida ambao ni muhimu ili kutoa nafasi kwa miti mingine kukua kwa wepesi).

Mfuko wa jamii ulianzishwa kwa vijiji tisa tu, saba vya Ulanga na viwili Wilaya ya Kilombero lakini pesa zilikuwa zinapitishiwa kwa shirika lisilolakiserikali liloko Ifakara. Shirika hilo lilikuwa na miradi yao na fedha za jamii za KVTC zilikuwa ni kama ziada kwao. Tuliendelea kupokea malalamiko zaidi kwamba miradi inayotekelezwa ni ya kiwango cha chini na kwamba kuna ufujaji wa fedha. Hivyo nilipewa kitengo cha jamii nikiendeshe, nilianza kwa kusikiliza malalamiko, halafu niliandaa mikutano na wanavijiji ili kuweza kutatua matatizo na malalamiko yaliyoko. Tuligundua mapungufu kwneye sekta ya elimu na afya hivyo tuliamua kuwekeza kwenye hizi sekta mbili kwa kutumia mfuko wa jamii. Tuliacha kupitishia hela kwenye NGO na kuanzisha akaunti ya benki inayosimamiwa na KVTC na wanakijiji kwenye kila kijiji. Kijiji kwa kupitia mikutano mkuu wanaamua na kukubaliana mradi wa kutekeleza, KVTC wanafanya tathimini na kama unaonekana kuwa na tija basi unapitishwa. Ili kuweza kupata fedha pande zote mbili lazima zisaini na ndipo mradi uendelee. Mfumo huu umekuwa ukiendelea vizuri na kuleta mapinduzi makubwa kwenye ufanisi na uwazi wa matumizi ya hela na aina ya miradi inayotekelezwa, na vijiji vimeongezeka kutoka tisa mpaka 17.